# Fungamana na Mwokozi kupitia Maagano na Ibada



MUHTASARI WA MAFUNZO KWA AJILI YA MABARAZA YA URATIBU YA ENEO, MISHENI, KIGINGI, KATA, NA TAWI

*Wakati wa mafunzo haya, utaona na kusikia uzoefu wa watoto wa Baba yetu wa Mbinguni katika sehemu tofauti tofauti wakiwa kwenye njia ya kufungamana na Mwokozi kupitia maagano na ibada. Utasikia jinsi upendo, kushiriki, na kualika kumewasaidia wao kuendelea katika njia ya agano kwa furaha. Unaweza kutambua jinsi gani kushiriki injili, kazi ya hekaluni na historia ya familia, na kuwajali wenye uhitaji vinavyochangia. Lakini juu ya yote, unaweza kugundua jinsi gani vitu hivi vyote "vinavyojumlishwa pamoja … katika Kristo" (Waefeso 1:10).*

## HATUA YA MAISHA 1: WATOTO



**Tazama video ya Rais Joy D. Jones na watoto, na kisha jadili ni nini mtakwenda na kufanya ili kuwasaidia watoto kujifunga wao wenyewe kwa Mwokozi kwenye njia ya agano.**

- Je, Roho alitufundisha nini wakati tukiangalia video hii?
- Je, ni kwa namna ipi kanuni za upendo, kushiriki, na kualika huwasaidia watoto wanapojitahidi kushiriki injili?
- Je, ni kwa namna ipi huduma huwasaidia watoto kubaki kwenye njia ya agano baada ya ubatizo?

## HATUA YA MAISHA 2: VIJANA

**Tazama video ya Rais Bonnie H. Cordon na Rais Stephen J. Lund na vijana, na kisha jadili ni nini mtakwenda na kufanya ili kuwasaidia vijana kujifunga wao wenyewe kwa Mwokozi kwenye njia ya agano.**

- Je, tunawezaje kuwasaidia vijana kuyashika maagano yao ya ubatizo na kujiandaa kwa hatua inayofuata kwenye njia ya agano?
- Je, ni kwa namna ipi kanuni za upendo, kushiriki, na kualika huwasaidia vijana kushiriki katika kazi ya hekaluni na historia ya familia?
- Je, tunawezaje kuwasaidia vijana kuhisi matumaini na kuhisi kuwa sehemu ya, wakati wanapokuwa wamefungwa kwa Mwokozi?

## HATUA YA MAISHA 3: VIJANA WAKUBWA

**Tazama video ya Rais Mark L. Pace na vijana wakubwa, na kisha jadili ni nini mtakwenda na kufanya ili kuwasaidia vijana wakubwa kujifunga wao wenyewe kwa Mwokozi kwenye njia ya agano.**

- Je, tunajifunza nini kutokana na upendo, kushiriki, na mwaliko ambao wengine hutupatia?
- Je, tunawezaje kuwasaidia vijana wakubwa kuhisi matumaini na kuwa sehemu ya, wakati wanapoongezeka katika kujitegemea na kuwatumikia wengine? Je, tunawezaje kuwasaidia kujua kwamba wao wanahitajika katika Kanisa la Bwana?
- Je, ni jukumu lipi kwa upande wa Kanisa na viongozi wanaojali hufanywa katika kuwaunganisha vijana wakubwa kwa Mwokozi?

## HATUA YA MAISHA 4: WATU WAZIMA

**Tazama video ya Rais Jean B. Bingham na watu wazima, na kisha jadili ni nini mtakwenda na kufanya ili kuwasaidia watu wazima kujifunga wao wenyewe kwa Mwokozi katika njia ya agano.**

- Je, maagano yetu huletaje uponyaji na kutusaidia kubakia kwenye njia—hata katika nyakati ngumu?
- Ni njia zipi ambazo tumezipata za kuwasaidia waumini pamoja na wengine kujifunga wao wenyewe kwa Mwokozi kupitia maagano na ibada?
- Ni kwa jinsi gani kukuza kujitegemea kwetu kiroho kunatusaidia sisi kupenda, kushiriki, na kualika?

NYENZO KWA AJILI YA MABARAZA YA URATIBU YA ENEO, MISHENI, KIGINGI, KATA, NA MATAWI

# Kwa ajili ya Watoto na Vijana

### MAELEZO YA JUMLA KWA WATOTO NA VIJANA

*Programu ya Watoto na Vijana imeundwa ili kuimarisha imani ya kizazi kinachoinukia katika Yesu Kristo, na kuwasaidia watoto, vijana, na familia zao kusonga mbele siku zote kwenye njia ya agano wakati wanapokabiliwa na changamoto za kimaisha. Huwasaidia watoto na vijana katika juhudi zao za kushiriki katika mkusanyiko wa Israeli na kazi ya wokovu na kuinuliwa katika maisha yao ya kila siku. Inalenga nyumbani na kusaidiwa na kanisa.*



## MATUMAINI KWA KIZAZI KINACHOINUKIA

Programu ya Watoto na Vijana husaidia kizazi kinachoinukia kukua katika njia nyingi, ikijumuisha kupitia ufunuo, uhuru wa kuchagua, na uhusiano. Watu binafsi hujifunza kupokea na kufanyia kazi ufunuo binafsi wanapotumia haki ya kujiamulia na kuchagua fursa za kukua kwa ajili yao wenyewe. Hii pia hutokea wakati vijana wanapojifunza kuongoza katika urais wa akidi na darasa. Wanajenga uhusiano na familia zao, viongozi wao, na wengine wa rika lao wanapofanya kazi na kuhudumu pamoja na kujua kwamba wao ni wa muhimu na wanahitajika katika kazi ya Bwana.

## JE, TUNAPASWA TUANZIE WAPI LEO?

Tunawaalika watoto, vijana, na wazazi wao na viongozi kujiwekea ahadi au kujiwekea tena ahadi ya kuwa kama Mwokozi kwa kushiriki katika kazi Yake. Juhudi hizi hazitakiwi kuwa ngumu! Hizi ni baadhi ya sehemu rahisi za kuanzia:

### Wazazi

- Ikusanye familia yako kwa ajili ya kujifunza injili. *Njoo, Unifuate* inaweza kusaidia. Unaweza kufikiria kuwa na majadiliano juu ya mada kama vile maagano, ufunuo, haki ya kujiamulia, na baraka za patriaki.
- Panga shughuli ya familia. Je, unawezaje kiusalama kumhudumia mtu katika mtaa au jumuiya yako? Kama, … JustServe hupatikana inaweza kukusaidia kupata mawazo ya hili.
- Kutana na kila mwana na binti. Jadili masilahi yao na ongea juu ya jinsi wanavyotaka kukua. Saidia na uwasaidie katika maendeleo binafsi. Ongea juu ya malengo gani wamejiwekea au wanataka kufanyia kazi.

### Viongozi wa Msingi

- Jua hali za nyumbani za watoto, na utafute ufunuo kuwasaidia kama watu binafsi.
- Anza kufanya mikutano ya Jumapili na shughuli za Msingi ana kwa ana au kimtandao (ikiwa ni salama na imeidhinishwa).
- Usijali kuhusu kuunganisha malengo ya watu binafsi na shughuli! Fokasi yako ni juu ya kuunganisha na kubariki watoto na familia zao—hususani pale wanapohitaji au kuomba msaada.

### Viongozi watu wazima wa vijana

- Anza kufanya mikutano ya Jumapili na akidi na shughuli za darasa ana kwa ana au kimtandao (ikiwa ni salama na imeidhinishwa). Watie moyo vijana kukariri na kuanza mikutano kwa kaulimbiu mpya ya darasa la Wasichana na akidi ya Ukuhani wa Haruni.
- Waite na watenge, uwezeshe urais wa akidi na wa darasa. Wasaidie kufanya mikutano ya mara kwa mara ya urais na kupanga na kuongoza mikutano ya Jumapili na shughuli. Fanyeni mabaraza ya vijana ya kata, na himiza ushiriki katika mikutano ya uratibu ya wamisionari na kazi za hekalu na historia ya familia. Shauri na saidia urais kadiri inavyowezekana bila ya wewe kuchukua nafasi yao. Saidia urais kujifunza stadi za uongozi kwa kutumia nyenzo za urais wa akidi na wa darasa.
- Panga na kufanya kambi za vijana na mkutano wa vijana kwa mwaka 2021, kwa kufuata miongozo ya usalama.
- Usijali kuhusu kuunganisha malengo ya watu binafsi na shughuli! Weka nguvu yako katika kuunganishwa na vijana wenyewe. Unaweza pia kusaidia urais wa akidi na wa darasa kuunganisha shughuli na mahitaji ya vijana.

KWA MAELEZO ZAIDI, ONA **CHILDRENANDYOUTH.CHURCHOFJESUSCHRIST.ORG**.

# Kwa ajili ya Watu Wazima

## SEHEMU ZA KUKUSANYIKA ZA VWW

Urais wa Kwanza umetoa idhini kwa maeneo ya kuanzisha maeneo ya kukusanyika kwa vijana wakubwa waseja kulingana na mahitaji ya eneo. Mahali pa kukusanyika ni mahali palipoteuliwa katika jengo lililopo (kama vile nyumba ya mkutano au jengo la chuo) ambapo vijana wakubwa waseja na marafiki zao wanaweza kukusanyika kushiriki katika baadhi au shughuli zote zifuatazo (kulingana na mahitaji ya sehemu husika na nyenzo):

- Elimu ya dini na kujifunza injili (ikiwemo chuo)
- Huduma na shughuli za kijamii
- Shughuli za hekalu na historia ya familia
- Fursa za kujitegemea na za kielimu
- Shughuli za umisionari na ufikiwaji wa jamii
- Programu nyingine za Kanisa



Sehemu zote za kukusanyika lazima ziidhinishwe na Urais wa Eneo na kusimamiwa na marais wa vigingi na maaskofu.

## MIITO KWA AJILI YA VIJANA WAKUBWA WASEJA NA WATU WAZIMA WASEJA

Mabadiliko ya sera ya hivi karibuni na ufafanuzi wake umesuluhisha hali ya uwezekano wa kutokuelewana na mila potofu kuhusu mipaka juu ya fursa kwa waumini waseja kuhudumu katika Kanisa la Bwana. Mabadiliko haya ya kisera na ufafanuzi, yaliyoidhinishwa na Urais wa Kwanza na Akidi ya Mitume Kumi na Wawili na kujumuishwa katika *Kitabu cha Maelezo ya Jumla*, huelezea kuwa vijana wakubwa waseja na watu wazima waseja wanaweza kubarikiwa na wanaweza kubariki wengine katika miito mingi, pamoja na kuwa viongozi wa kigingi na kata. Sera hizo hizo sasa zinafanya kazi katika vitengo vyote vya Kanisa, pamoja na vitengo vya vijana wakubwa waseja na watu wazima. Vizuizi dhidi ya vijana wakubwa waseja na watu wazima waseja kuhudumu katika urais wa kigingi, uaskofu, na urais wa kigingi wa Muungano wa Usaidizi wa Akina Mama katika vitengo vya vijana wakubwa waseja na watu wazima waseja vimeondolewa.

Waumini wasio na wenzi wanaweza kutumikia katika nafasi za uongozi ikiwa ni pamoja na urais wa kata na kigingi, urais wa akidi ya wazee, washauri wa uaskofu, wajumbe wa baraza, na washauri wa urais wa kigingi.

# Kuhitaji na Kukaribisha—Upendo, Shiriki, na Kualika

Wakati waumini wanapopambana kuhisi hali ya kukubalika, wakati mwingine viongozi na wengine bila kukusudia wanasema mambo ambayo huimarisha imani ya waumini hawa kwamba hawastahihili au hawahitajiki.

Kukumbuka kweli hizi juu ya upendo, kushiriki, na kualika kunaweza kusaidia katika kuwakaribisha wote kwenye shughuli, ushirika, na kuwa mali ya Kanisa la Yesu Kristo:

- Kila mtu ni mtoto mpendwa wa Mungu aliye na asili na hatima ya kiungu. Mbali na baraka za milele anazoahidi kwa waaminifu, anataka kuwabariki watoto wake sasa, wakati wa maisha haya.
- Kila mtoto wa Mungu anahitajika katika kazi ya kujenga ufalme Wake.
- Ili kumsaidia mtu kuhisi yeye ni mali ya, na anahitajika, anza na upendo. Sikiliza kuelewa uzoefu wake. Usifikirie kuwa tayari unajua au anaelewa.
- Hatuna majibu ya maswali yote ambayo sisi au wengine tunakabiliwa nayo katika maisha haya. Kwa mfano, sisi hatujui sababu ambazo mtu anaweza kuwa anakabiliwa na changamoto fulani.



- Kuwa muwazi na usihukumu. Mkaribishe kila mtu, popote mtu huyo alipo katika safari yake. Jitolee kusaidia na zingatia ukweli kwamba kila mtu anahitajika katika Kanisa.
- Ikiwa unasema bila kukusudia jambo lenye kuumiza, usijitetee; omba radhi kisha utafute msamaha na uboreshaji.

KWA HABARI JUU YA KUWASAIDIA WAUMINI WALIO KATIKA HALI MAALUM, ONA COUNSELINGRESOURCES.CHURCHOFJESUSCHRIST.ORG

## INASAIDIA KUSEMA

- Karibu! Unahitajika na unapendwa. Asante kwa kuwa hapa.
- Nifundishe kuhusu uzoefu wako. Ungependa mimi nielewe nini?
- Tunakukaribisha na tunakuhitaji popote ulipo katika safari yako. Tunawezaje kusaidia? Unawezaje kutusaidia sisi?
- Mungu anataka ufurahi sasa. Injili Yake inatoa matumaini na furaha kwa watoto Wake wote.

KANISA LA YESU KRISTO LA WATAKATIFU WA SIKU ZA MWISHO


© 2021 by Intellectual Reserve, Inc. All rights reserved. Toleo: 3/21. PD60012741 000. Kimepigwa chapa Marekani